

# Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote

**Kitovu** cha Malengo ya Maendeleo Endelevu

### LENGO NAMBA 1
## Kutokomeza umasikini
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia kuvunja mzunguko wa umasikini pamoja na ulemavu.

### LENGO NAMBA 2
## Kukomesha Njaa
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote huhakikisha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wananufaika na mipango ya lishe katika shule.

### LENGO NAMBA 3
## Afya
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia kukabiliana na ubaguzi dhidi ya wanafunzi wenye ulemavu, kuwawezesha kukusanyika na wenzao,kukuza ustawi wao na kufanya maamuzi sahihi kuhusu afya zao.

### LENGO NAMBA 4
## Elimu
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote huhakikisha kuwepo kwa usawa katika upatikanaji wa elimu bora kwa wote na hukuza utoaji wa fursa za kujifunza muda wote maishani kwa wanafunzi wenye ulemavu.

### LENGO NAMBA 5
## Usawa wa kijinsia
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wasichana wenye ulemavu, ambao mara nyingi hukabiliwa na ubaguzi maradufu.

### LENGO NAMBA 6
## Maji safi na usafi
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote ina maana kwamba wanafunzi wenye ulemavu wataweza kujifunza na hatimaye kuwa na mazoea bora ya matumizi ya maji, mazoea bora ya usafi wa mwili na mazoea bora ya usafi wa kimazingira.

### LENGO NAMBA 7
## Nishati kwa wote
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote ina maana kwamba wanafunzi wenye ulemavu wanaweza kujifunza na kufanya maamuzi sahihi kuhusu uhifadhi wa nishati na vyanzo vya nishati mbadala.

### LENGO NAMBA 8
## Ajira bora / Kazi zenye staha
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote hukuza kujiamini, ujuzi katika ujasiriamali na uvumbuzi, na kuendeleza uzalishaji wa fursa za ajira.

### LENGO NAMBA 9
## Viwanda, ubunifu na miundombinu
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote hukuza ujuzi na stadi zinazotakiwa katika kujenga miundombinu iliyo imara, endelevu na inayofikika.

### LENGO NAMBA 10
## Kupunguza tofauti
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote huleta mabadiliko katika tofauti za kijamii na kiuchumi na kuleta usawa kwa wanafunzi wote katika kuzifikia shule na kupata msaada sahihi.

### LENGO NAMBA 11
## Miji na jamii endelevu
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia wanafunzi wenye ulemavu kuhakikisha kwamba miji na jamii vinafikika, vinakuwa jumuishi na salama.

### LENGO NAMBA 12
## Matumizi na uzalishaji wenye uwajibikaji
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wanaelewa kuhusu ufumbuzi (wa matatizo) /masuluhisho na matumizi endelevu.

### LENGO NAMBA 13
## Kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote inatoa nafasi kwa wanafunzi wenye ulemavu kushirikishwa katika majadiliano ya (ndani) kitaifa na kuchukua hatua juu ya athari za mabadiliko ya tabia nchi.

### LENGO NAMBA 14
## Uhai katika maji
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote husaidia kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wanaelewa jinsi ya kuhifadhi na kutumia bahari kwa maendeleo endelevu.

### LENGO NAMBA 15
## Uhai katika ardhi
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote huwaongezea wanafunzi wenye ulemavu maarifa kuhusu ujuzi/stadi kwa ajili ya harakati endelevu za kimaisha/kikazi na maisha ya kujitegemea.

### LENGO NAMBA 16
## Amani, haki na taasisi madhubuti
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote ni muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa jamii jumuishi, zenye haki pamoja na kupunguza unyanyapaa, mawazo potofu na ubaguzi.

### LENGO NAMBA 17
## Ushirikiano katika kufanikisha malengo
Elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote huwa na mafanikio kunapokuwa na ushirikiano imara kati ya serikali, wizara na asasi za kiraia ikiwa ni pamoja na wazazi na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu.

Vyanzo: ICSU na ISSC, 2015; GEMR, 2016
Picha © Sightsavers 2015/Peter Caton

Dunia bora **kwa kila mmoja.**

www.iddcconsortium.net/what-we-do/post-2015

International Disability and Development Consortium

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS

# Utekelezaji wa **elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote katika lengo namba 4 la maendeleo endelevu**

4 ELIMU BORA

### SHABAHA 4.b
**Misaada ya masomo**

Kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wanakuwa na fursa sawa za kupata misaada ya masomo ya elimu ya juu ambayo huandaliwa kwa ajili ya nchi zinazoendelea.

Image © Liliane Foundation



### SHABAHA 4.c
**Walimu**

Kuongeza usambazaji wa walimu wenye sifa stahili ambao wamehitimu mafunzo ya mbinu jumuishi za ufundishaji.

Image © Julia McGeown, Handicap International



### SHABAHA 4.1
**Elimu ya msingi na sekondari**

Kusaidia Wizara za Elimu katika kuendeleza mitaala na tathmini jumuishi katika kufuatilia wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu.

Image © Mission East



### SHABAHA 4.a
**Vifaa vya elimu na mazingira ya kujifunzia**

Kujenga na kuimarisha nyenzo na vifaa vya elimu kwa kuzingatia mahitaji ya watoto, jinsia, na ulemavu na kuweka mazingira jumuishi yaliyo salama, yasiyo na vurugu na yenye ufanisi kwa wote.

Image © Sightsavers



### SHABAHA 4.2
**Elimu ya awali na malezi**

Kuhakikisha kwamba watoto wa umri wa chini ya miaka mitano wenye ulemavu wanajumuishwa katika mipango ya maendeleo inayoshughulikia malezi ya watoto.

Image © Leonard Cheshire Disability Hamish Roberts



## LENGO LA 4:

## Kuhakikisha elimu mjumuisho yenye haki na usawa kwa wote na kukuza utoaji wa fursa za kujifunza muda wote maishani kwa wote



### SHABAHA 4.7
**Maendeleo endelevu na uraia wa kimataifa/ ulimwengu**

Kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wenye ulemavu wanapata maarifa na ujuzi wa kuelewa maendeleo endelevu na uraia wa kimataifa/ ulimwengu.

Image © Plan International



### SHABAHA 4.3
**Ufundi, ufundi stadi na elimu ya juu, pamoja na vyuo vikuu**

Kusaidia taasisi za elimu ya juu na vituo vya mafunzo ya amali (ufundi) katika kuwajumuisha wanafunzi wenye ulemavu.

Image © Light for the world







### SHABAHA 4.6
**Kujua kusoma, kuandika na kuhesabu**

Kuhakikisha kwamba wanafunzi wenye ulemavu wanaweza kusoma, kuandika na kuhesabu kufikia uwezo wao wote (wa kujifunza), kwa kutumia muundo wanaouweza (kama vile vitabu vyenye muundo rahisi kusoma, maandishi ya nukta nundu, machapisho makubwa, picha na kadhalika) na lugha ya alama.

Image © Julia McGeown, Handicap International

### SHABAHA 4.5
**Tofauti**

Kuhakikisha kwamba Mfumo wa Habari za Uongozi wa Elimu katika shule unaonesha mgawanyo wa taarifa za ulemavu na kiwango chake.

Image © Sightsavers

### SHABAHA 4.4
**Stadi za ajira**

Kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu, ili kuwawezesha kuendeleza ujuzi/stadi zifaazo kwa ajili ya kazi (ajira).

Image © CBM Australia

Dunia bora **kwa kila mmoja.**

www.iddcconsortium.net/what-we-do/post-2015

International Disability and Development Consortium

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS